# SHERIA YA MAREKEBISHO YA KUMI YA KATIBA YA ZANZIBAR YA 1984

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


**SEHEMU YA KWANZA**
**UTANGULIZI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Kusomwa.

**SEHEMU YA PILI**
**MAREKEBISHO MBALI MBALI**

3. Marekebisho ya kifungu cha 1.
4. Marekebisho ya kifungu cha 2.
5. Kuongeza kifungu kipya cha 2A.
6. Marekebisho ya kifungu cha 9.
7. Marekebisho ya kifungu cha 10.
8. Marekebisho ya kifungu cha 12.
9. Marekebisho ya kifungu cha 24.
10. Marekebisho ya kifungu cha 25A.
11. Marekebisho ya kifungu cha 26.
12. Marekebisho ya kifungu cha 27.
13. Marekebisho ya kifungu cha 28.
14. Marekebisho ya kifungu cha 29.
15. Marekebisho ya kifungu cha 30.
16. Marekebisho ya kifungu cha 32.

17. Marekebisho ya kifungu cha 33.
18. Marekebisho ya kifungu cha 34.
19. Marekebisho ya kifungu cha 37.
20. Marekebisho ya kichwa cha maneno.
21. Marekebisho ya kifungu cha 39.
22. Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 39A .
23. Marekebisho ya kifungu cha 40.
24. Marekebisho ya kifungu cha 41.
25. Marekebisho ya kifungu cha 42.
26. Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 42A.
27. Marekebisho ya kifungu cha 43.
28. Marekebisho ya kifungu cha 44.
29. Marekebisho ya kifungu cha 45.
30. Marekebisho ya kifungu cha 46.
31. Marekebisho ya kifungu cha 47.
32. Marekebisho ya kifungu cha 48.
33. Marekebisho ya kifungu cha 49.
34. Marekebisho ya kifungu cha 50.
35. Marekebisho ya kifungu cha 54.
36. Marekebisho ya kifungu cha 57.
37. Marekebisho ya kifungu cha 61.
38. Marekebisho ya kichwa cha maneno.
39. Marekebisho ya kifungu cha 63.

40. Marekebisho ya kifungu cha 64.
41. Marekebisho ya kifungu cha 66.
42. Marekebisho ya kifungu cha 67.
43. Marekebisho ya kifungu cha 72.
44. Marekebisho ya kifungu cha 73.
45. Marekebisho ya kifungu cha 74.
46. Marekebisho ya kifungu cha 78.
47. Marekebisho ya kifungu cha 79.
48. Kuongeza kifungu kipya cha 80A..
49. Marekebisho ya kifungu cha 81.
50. Marekebisho ya kifungu cha 84.
51. Marekebisho ya kifungu cha 86.
52. Marekebisho ya kifungu cha 91.
53. Marekebisho ya kifungu cha 92.
54. Marekebisho ya kifungu cha 96.
55. Marekebisho ya kifungu cha 99A.
56. Marekebisho ya kifungu cha 102.
57. Marekebisho ya kichwa cha maneno.
58. Marekebisho ya kifungu cha 116.
59. Marekebisho ya kifungu cha 117.
60. Marekebisho ya kifungu cha 118.
61. Marekebisho ya kifungu cha 120.
62. Marekebisho ya kifungu cha 121.
63. Marekebisho ya kifungu cha 122.
64. Marekebisho ya kifungu cha 124.
65. Marekebisho ya kifungu cha 128.
66 Marekebisho ya kifungu cha 129.
67. Marekebisho ya kifungu cha 134.

**SHERIA NAM. 9 YA 2010**
**NIMEKUBALI**

{ AMANI ABEID KARUME }
**RAIS WA ZANZIBAR**
**NA**
**MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI**

13 AGOSTI, 2010

# SHERIA YA MAREKEBISHO YA KUMI YA KATIBA YA ZANZIBAR YA 1984

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajuilikana kama Sheria ya Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar ya 2010 na itaanza kutumika mara itakapotiwa saini na Rais.

Kusomwa.

**2.** Sheria hii itasomwa pamoja na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambapo katika Sheria hii itajulikana kama "Katiba".

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO MBALI MBALI

Marekebisho ya kifungu cha 1.

**3.** Kifungu cha 1 cha Katiba kinafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

"Zanzibar na mipaka yake.

**1.** Zanzibar ni Nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na Visiwa vidogo vilivyoizunguka na bahari yake ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar."

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**4.** Kifungu cha 2 cha Katiba kinafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

"Zanzibar na Muungano.

**2.** Zanzibar ni miongoni mwa Nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania."

Kuongeza kifungu kipya cha 2A.

**5.** Katiba inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 2A mara baada ya kifungu cha 2 kama ifuatavyo:-

"Mikoa na Wilaya za Zanzibar.

**2A.** Kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Serikali, Rais aweza kuigawa Zanzibar katika Mikoa, Wilaya na maeneo mengineyo kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi."

Marekebisho ya kifungu cha 9.

**6.** Kifungu cha 9(3) cha Katiba kinarekebishwa kwa kufuta maneno "pamoja" yaliyopo baina ya maneno "Zanzibar" na "na" na badala yake kuweka maneno "utakuwa wa Umoja wa Kitaifa."

Marekebisho ya kifungu cha 10.

**7.** Kifungu cha 10 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

(i) kwa kufuta kijifungu cha (3) na kukiandika upya kama ifuatavyo:

"(3) Kusimamia Maendeleo ya Uchumi wa Nchi kufuatana na misingi na madhumuni yaliyowekwa na Katiba, kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora, kuratibu na kusimamia uendeshaji wa rasilimali muhimu za Nchi."

(ii) kwa kufuta neno "Itatoa" liliopo mwanzo wa kijifungu cha (4) na kuweka badala yake "Kutoa" na kufuta maneno "wake katika Katiba" yaliyopo baina ya neno "muongozo" na "kuhakikisha".

(iii) kwa kufuta maneno "katika kutekeleza siasa hiyo" yaliopo mwanzo wa kijifungu cha (5).

(iv) kwa kufuta maneno "italenga siasa yake katika" yaliopo mwanzo wa kijifungu cha (6) na kufuta neno "madaraka" liliopo baina ya neno "katika" na "yote" na kuweka badala yake neno "madaraja".

Marekebisho ya kifungu cha 12.

**8.** Kifungu cha 12(5) cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza neno "ulemavu" baina ya neno "jinsia" na "pahala walipotokea".

Marekebisho ya kifungu cha 24.

**9.** Kifungu cha 24(3) cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta neno "Maombi" liliopo mwanzo wa kijifungu na kuweka badala yake neno "Rufaa" na kwa kuongeza maneno "na uamuzi wao utakuwa ni wa mwisho na hautokatiwa rufaa kwenye Mahkama ya Rufaa ya Tanzania" mwisho wa kijifungu.

Marekebisho ya kifungu cha 25A.

**10.** Kifungu cha 25A cha Katiba kinafanywa marekebisho kwa kuongeza kijifungu cha (2) kama ifuatavyo:-

"(2) Rufaa dhidi ya uwamuzi wa Mahkama Kuu katika shauri lililofunguliwa dhidi ya masharti ya kifungu hiki itasikilizwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 24(3) cha Katiba."

Marekebisho ya kifungu cha 26.

**11.** Kifungu cha 26(1) cha Katiba kinafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

"Afisi ya Rais na sifa za kuchaguliwa kuwa Rais.

**26.**(1) Kutakuwa na Rais wa Zanzibar ambaye atakuwa Mkuu wa Nchi ya Zanzibar, Kiongozi Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi."

Marekebisho ya kifungu cha 27.

**12.** Kifungu cha 27 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta kijifungu cha (3) na kukifanya kijifungu cha (4) kuwa cha (3).

Marekebisho ya kifungu cha 28.

**13.** Kifungu cha 28 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

(i) katika kijifungu cha (1) kwa:

(a) kuongeza neno "au" katika kila mwisho wa aya (a), (b), (c) na (d);

(b) kufuta maneno "na kukubalika" yaliyopo katika aya (c); na

(c) kufuta aya (e) na kuifanya aya (f) kuwa (e).

(ii) katika kijifungu cha (3) kwa kufuta neno "mfululizo".

Marekebisho ya kifungu cha 29.

**14.** Kifungu cha 29 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza maneno "Jamhuri ya Muungano wa" mara tu baada ya neno "Ikiwa" na kufuta maneno "ambapo Zanzibar pia inahusika" yaliopo baina ya maneno "vita" na "na".

Marekebisho ya kifungu cha 30.

**15.** Kifungu cha 30(1)(b) cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta neno "mfululizo" liliopo baina ya maneno "viwili" na "vilivyokwisha".

Marekebisho ya kifungu cha 32.

**16.** Kifungu cha 32(2)(c) cha Katiba kinafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

> "**32.**(2)(c) Jaji Mkuu atathibitisha kwa kadri aonavyo baada ya kuitafakari ripoti ya Kamati na atapeleka hati ya uthibitisho kwamba Rais hawezi kumudu kufanya kazi zake kutokana na maradhi ya kimwili au akili kwa Baraza la Mapinduzi na kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi; na iwapo Jaji Mkuu hatabatilisha uthibitisho wake ndani ya siku saba kutokana na Rais kupata nafuu na kurejea kazini, basi itahesabiwa kwamba kiti cha Rais kiwazi kwa mujibu wa kifungu 33(1)(c) cha Katiba na masharti yaliyomo katika kifungu cha 34(1) cha Katiba yatatumika."

Marekebisho ya kifungu cha 33.

**17.** Kifungu cha 33 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

(i) kwa kufuta kijifungu cha (1) na kukiandika upya kama ifuatavyo:

(1) Endapo kiti cha Rais kitakuwa wazi kwa:

(a) kufariki; au

(b) kujiuzulu; au

(c) maradhi ya kimwili au kiakili; au

(d) sababu nyengine yoyote itakayomfanya Rais kushindwa kutekeleza kazi za Rais."

watu wafuatao, kwa mujibu wa mpangilio watashika nafasi hiyo:

(i) Makamo wa Pili wa Rais au ikiwa hayupo;

(ii) Spika wa Baraza la Wawakilishi ambaye anatoka katika chama anachotoka Rais na yeye ikiwa hayupo;

(iii) Jaji Mkuu wa Zanzibar.

(ii) kwa kufuta maneno "Waziri Kiongozi" na badala yake kuweka maneno "Makamo wa Pili wa Rais" katika kijifungu cha (2)(b)(i).

(iii) kwa kufuta kijifungu cha (2)(b)(ii) na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

"(iii) Mjumbe yeyote wa Baraza la Mapinduzi ambaye Rais ataona anafaa."

Marekebisho ya kifungu cha 34.

**18.** Kifungu cha 34 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

(i) kwa kuongeza maneno "kwa mujibu wa kifungu cha 33(1) cha Katiba" baina ya maneno "madaraka" na "atachukua" katika aya ya (i) ya kijifungu cha (1).

(ii) kwa kufuta maneno "Waziri Kiongozi" na kuweka badala yake "Makamo wa Pili wa Rais" na kwa kufuta maneno "Baraza la" yaliyopo baina ya "Mawaziri" na "Makamo wa Pili wa Rais" katika kijifungu cha (1) aya (iii).

(iii) na kwa kuongeza aya mpya ya (iv) katika kijifungu cha (1) kama ifuatavyo:

"(iv) Bila ya kujali masharti ya vifungu vya 28(3) na 30(1)(b) vya Katiba, endapo mtu anaemfuata Rais kwa madaraka atashika kiti cha Rais kwa kipindi kinachopungua miaka minne ataruhusiwa kugombea nafasi ya Rais mara mbili, lakini kama atashika kiti cha Rais kwa muda wa miaka minne au zaidi ataruhusiwa kugombea nafasi ya Rais mara moja tu."

Marekebisho ya kifungu cha 37.

**19.** Kifungu cha 37(2) cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta maneno "au amekuwa na mwenendo unaodhalilisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar" yaliyopo baina ya neno "Katiba" na neno "na" na kuweka badala yake maneno "au amekuwa na mwenendo unaodhalilisha kiti cha Rais".

Marekebisho ya kichwa cha maneno.

**20.** Kichwa cha maneno katika Sehemu ya Pili kiliopo baina ya kifungu cha 38 na 39 kinarekebishwa kwa kufuta maneno "Waziri Kiongozi" na badala yake kuweka maneno "Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais".

Marekebisho ya kifungu cha 39.

**21.** Kifungu cha 39 cha Katiba kinafutwa na badala yake kinaandikwa upya kama ifuatavyo:-

"Makamo Wawili wa Rais.

**39.**(1) Kutakuwa na Makamo Wawili wa Rais ambao watajuilikana kama Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais.

(2) Ndani ya siku saba mara baada ya kushika madaraka, Rais atateua Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais.

(3) Makamo wa Kwanza wa Rais atatakiwa awe na sifa za kumuwezesha kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na atateuliwa na Rais baada ya kushauriana na chama kilichotokea nafasi ya pili katika matokeo ya kura ya Uchaguzi wa Rais.

Isipokuwa kwamba:-

(i) iwapo chama kilichotokea nafasi ya pili katika matokeo ya kura ya uchaguzi wa Rais kimepata chini ya asilimia kumi (10%) ya kura zote za uchaguzi wa Rais; au

(ii) endapo Rais atakuwa hana mpinzani katika uchaguzi,

basi nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais itapewa chama chochote cha upinzani kilichotokea cha pili kwa wingi wa viti vya Majimbo katika Baraza la Wawakilishi.

(4) Makamo wa Kwanza wa Rais hatokuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(5) Makamo wa Kwanza wa Rais atakuwa ni Mshauri Mkuu wa Rais katika kutekeleza kazi zake na atafanya kazi zote atakazopangiwa na Rais.

(6) Makamo wa Pili wa Rais atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka katika chama anachotoka Rais.

(7) Makamo wa Pili wa Rais atakuwa ndiye Mshauri Mkuu wa Rais katika kutekeleza kazi zake na pia atakuwa ndiye Kiongozi wa shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi.

(8) Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili wa Rais hawatoanza kazi mpaka waapishwe kiapo cha uaminifu na kiapo chengine mbele ya Rais kama kitakavyoelezwa katika Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(9) Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais wakati wote watakapokuwa madarakani watawajibika kwa Rais."

Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 39A.

**22.** Katiba inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 39A mara baada ya kifungu cha 39 kama ifuatavyo:-

"Kuachwa wazi kwa nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

**39A.**(1) Endapo, ndani ya siku saba mara baada ya Rais kushika madaraka, chama kinachositahiki kutoa Makamo wa Kwanza wa Rais kitashindwa kuwasilisha kwa Rais jina la uteuzi wa Makamo wa Kwanza wa Rais;

Rais bila ya kujali masharti ya kifungu cha 39(1) na (3) cha Katiba, atawacha wazi nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na kuteua Makamo wa Pili wa Rais.

(2) Kwa mujibu wa masharti ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki, Rais, bila ya kujali masharti ya kifungu cha 42 (2) cha Katiba, atateua Mawaziri na kuwacha wazi nafasi za uteuzi wa chama au vyama vya upinzani."

Marekebisho ya kifungu cha 40.

**23.** Kifungu cha 40 cha Katiba kinafutwa na badala yake kinaandikwa upya kama ifuatavyo:-

"Kuwa wazi kwa nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais.

**40.**(1) Endapo nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais itakuwa wazi:

(a) kwa sababu ya kufariki au kujiuzulu; au

(b) ikiwa Rais amefuta uteuzi huo; au

(c) kwa sababu nyengine yeyote itakayomfanya ashindwe kuwa na sifa za Makamo wa Kwanza au Makamo wa Pili wa Rais, Rais atamteua Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais kutegemeana na nafasi iliyo wazi.

(2) Iwapo mtu atafutwa katika nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mujibu wa kijifungu cha (1)(b) cha kifungu hiki, chama chake si zaidi ya siku kumi na nne kitapendekeza kwa Rais jina la mtu mwengine."

Marekebisho ya kifungu cha 41.

**24.** Kifungu cha 41 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:

(i) kwa kufuta maneno "Waziri Kiongozi" kila yanapojitokeza katika kijifungu cha (1), (2), (3), (5), (6) na (7)(i) na badala yake kuweka maneno "Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais";

(ii) kwa kufuta maneno "Waziri Kiongozi" katika kijifungu (7)(ii) na badala yake kuweka maneno "Makamo wa Pili wa Rais".

Marekebisho ya kifungu cha 42.

**25.** Kifungu cha 42 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta kijifungu cha (2) na badala yake kuweka chengine kipya kama ifuatavyo:-

"(2) Rais ndani ya kipindi cha siku kumi na nne mara baada ya kuteua Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais, kwa kushauriana na Makamo wote Wawili wa Rais atateua Mawaziri kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuzingatia uwiano wa viti vya majimbo kwa vyama vya siasa vilivyomo ndani ya Baraza la Wawakilishi."

Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 42A

**26.** Katiba inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 42A mara baada ya kifungu cha 42 kama ifuatavyo:-

"Kuacha kufanya kazi kwa Makamo wa Kwanza na Mawaziri.

**42A.** Endapo Makamo wa Kwanza wa Rais na, au Mawaziri kutoka vyama vya upinzani watajiuzulu au wataacha kutekeleza kazi zao kwa zaidi ya siku saba, Rais bila ya kujali masharti ya vifungu vya 39(3) na 42(2) vya Katiba, atawacha wazi nafasi za uteuzi wao; na iwapo nafasi hizo zitakuwa wazi kwa zaidi ya siku tisini, Rais anaweza kuteuwa Mawaziri wengine kujaza nafasi zao."

Marekebisho ya kifungu cha 43.

**27.** Kifungu cha 43 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

(i) kwa kufuta maneno "Waziri Kiongozi" katika kijifungu cha (1), (4)(b) na (6)(a) na badala yake kuweka maneno "Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais"; na

(ii) kwa kufuta kijifungu cha (5) na kuweka kipya kama ifuatavyo:

"(5) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndiyo itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za Serikali kwa ujumla, na Mawaziri chini ya uongozi wa Makamo wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar".

Marekebisho ya kifungu cha 44.

**28.** Kifungu cha 44(1) cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta maneno "Waziri Kiongozi" na badala yake kuweka maneno "Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais".

Marekebisho ya kifungu cha 45.

**29.** Kifungu cha 45(1) na (2) cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta maneno "Waziri Kiongozi" na badala yake kuweka maneno "Makamo wa Pili wa Rais".

Marekebisho ya kifungu cha 46.

**30.** Kifungu cha 46 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta maneno "ale kiapo" na kuweka badala yake "aapishwe" na kuongeza maneno "mbele ya Rais" baina ya maneno "zake" na "kama".

Marekebisho ya kifungu cha 47.

**31.** Kifungu cha 47 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta maneno "Waziri Kiongozi" na badala yake kuweka maneno "Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais" na kufuta maneno "wale kiapo" yaliyopo baina ya maneno "kwanza" na "cha" na kuweka badala yake neno "waapishwe" na kuongeza maneno "mbele ya Rais" baina ya maneno "zao" na "kama".

Marekebisho ya kifungu cha 48.

**32.** Kifungu cha 48 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

(i) kwa kufuta neno "Serikali" na badala yake kuweka neno "Rais" katika aya (a); na

(ii) kwa kufuta aya (d) na badala yake kuweka aya ya (d) mpya kama ifuatavyo:

"(d) mara baada ya Rais kushika madaraka."

Marekebisho ya kifungu cha 49.

**33.** Kifungu cha 49 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

(i) kwa kuongeza maneno "ambaye atakuwa pia Katibu Mkuu Kiongozi" baina ya maneno "Baraza la Mapinduzi" na "ataeteuliwa" katika kijifungu cha (1); na

(ii) kwa kufuta kijifungu cha (2) na kukiandika upya kama ifuatavyo:

"(2) Katibu Mkuu Kiongozi atakuwa ndiye kiongozi wa utumishi wa umma kwa Zanzibar na hatoanza kazi zake mpaka atakapoapishwa na Rais."

Marekebisho ya kifungu cha 50.

**34.** Kifungu cha 50 cha Katiba kinafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

"Katibu Mkuu.

**50.**(1) Pale Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais au Waziri yeyote mwengine anapokuwa na dhamana ya Wizara yeyote ya Serikali, atakuwa ndiye kiongozi na Msimamizi Mkuu na bila ya kuathiri masharti yoyote ya usimamizi, Katibu Mkuu ambaye afisi yake itakuwa ni ya utumishi wa Serikali atakuwa ndiye Afisa Mtendaji Mkuu wa Wizara.

(2) Kutakuwa na Katibu Mkuu katika Afisi ya Rais, Katibu Mkuu katika Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Katibu Mkuu katika Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais na Makatibu Wakuu wengine wa Wizara mbalimbali kama Rais atakavyoona inafaa.

(3) Makatibu Wakuu waliotajwa kwenye kijifungu cha (2) cha kifungu hiki watateuliwa na Rais.

(4) Rais anaweza kuteua Naibu Katibu Mkuu wa Wizara.

(5) Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu yeyote hatoanza kazi yake mpaka kwanza aapishwe kiapo cha uaminifu na kiapo chengine chochote cha utendaji wa kazi zake mbele ya Rais kama kitavyowekwa na Baraza la Wawakilishi."

Marekebisho ya kifungu cha 54.

**35.** Kifungu cha 54(2) cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta maneno "Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, Chuo cha Mfunzo, Jeshi la Kujenga Uchumi" na badala yake kuweka maneno "Idara Maalum."

Marekebisho ya kifungu cha 57.

**36.** Kifungu cha 57 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta maneno "ale kiapo" na kuweka badala yake "aapishwe" na kwa kuongeza maneno "mbele ya Rais" baina ya maneno "zake" na "kama".

Marekebisho ya kifungu cha 61.

**37.** Kifungu cha 61 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

(i) kwa kufuta maneno "kwa kushauriana na Rais wa Jamhuri ya Muungano" yaliyopo kwenye kijifungu cha (1).

(ii) kwa kufuta maneno "ale kiapo" na kuweka badala yake "aapishwe" na kwa kuongeza maneno "mbele ya Rais" mwisho wa maneno katika kijifungu cha (3).

Marekebisho ya kichwa cha maneno.

**38.** Kichwa cha maneno cha Sura ya Tano kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta maneno "Muundo wa Baraza la Wawakilishi" na kuweka badala yake "Muundo wa Baraza la Kutunga Sheria".

Marekebisho ya kifungu cha 63.

**39.** Kifungu cha 63(2) cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta maneno "Baraza la Wawakilishi" yaliopo baina ya neno "za" na "basi" na kuweka badala yake maneno "Baraza la Kutunga Sheria".

Marekebisho ya kifungu cha 64.

**40.** Kifungu cha 64 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta aya (d) na kuiandika aya mpya ya (d) kama ifuatavyo:-

(d) Spika iwapo hatakuwa amechaguliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi"

Marekebisho ya kifungu cha 66.

**41.** Kifungu cha 66 cha Katiba kinafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

"Wajumbe wa kuteuliwa.

**66.** Kutakuwa na Wajumbe kumi wa kuteuliwa wa Baraza la Wawakilishi ambao watateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa zilizoelezwa na kifungu cha 68(a) na (c) cha Katiba ambao wakiteuliwa watafaa kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Isipokuwa kwamba Wajumbe wasiopungua wawili watateuliwa na Rais kwa kushauriana na Kiongozi wa Upinzani katika Baraza la Wawakilishi au kwa kushauriana na Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi ndani ya Baraza la Wawakilishi iwapo hakuna Kiongozi wa Upinzani."

Marekebisho ya kifungu cha 67.

**42.** Kifungu cha 67(1) cha Katiba kinarekebishwa kwa kufuta maneno "thelathini (30%)" na badala yake kuweka maneno "arobaini (40%)".

Marekebisho ya kifungu cha 72.

**43.** Kifungu cha 72(2) cha Katiba kinarekebishwa kwa kufuta maneno "wawe miongoni mwa watu wenye uzoefu".

Marekebisho ya kifungu cha 73.

**44.** Kifungu cha 73(2) cha Katiba kinarekebishwa kwa kufuta neno "Memba" na badala yake kuweka neno "Mjumbe", kufuta maneno "Waziri Kiongozi" na badala yake kuweka maneno "Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais" na kufuta maneno "Mkuu wa Mkoa".

Marekebisho ya kifungu cha 74.

**45.** Kifungu cha 74 cha Katiba kinarekebishwa kama ifuatavyo:-

(i) kwa kufuta maneno "Waziri Kiongozi" na badala yake kuweka maneno "Makamo wa Pili wa Rais" na kufuta maneno "Mkuu wa Mkoa" katika kijifungu cha (1); na

(ii) kwa kufuta aya (b) ya kijifungu cha (3) na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

"(b) ikiwa amechaguliwa kuwa Rais, Makamo wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais, Waziri, Naibu Waziri, Mkuu wa Mkoa au Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi."

Marekebisho ya kifungu cha 78.

**46.** Kifungu cha 78 cha Katiba kinarekebishwa kwa kufuta kijifungu cha (3) na kukiandika upya kama ifuatavyo:-

"(3) Wakati Muswada umepitishwa na Baraza la Wawakilishi, Spika ataupeleka kwa Rais ndani ya siku thelathini kupata kibali chake."

Marekebisho ya kifungu cha 79.

**47.** Kifungu cha 79 cha Katiba kinarekebishwa kama ifuatavyo:-

(i) kuongeza maneno "ndani ya kipindi cha siku tisini" baada ya maneno "anaweza" na "ama" katika kijifungu cha (1); na

(ii) kuongeza vijifungu vipya vya (2) na (3) mara baada ya kijifungu cha (1) kama ifuatavyo na kuvifanya vijifungu vya (2), (3) na (4) kuwa (4), (5) na (6):

"(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 62 (3) cha Katiba mara baada ya siku tisini tokea siku ya kuwasilishwa Mswada kwa Rais kumalizika bila ya kukubaliwa au kukataliwa na Rais, Mswada huo utachukuliwa kuwa ni Sheria.

(3) Endapo itatokea Mswada kuwa Sheria chini masharti ya kijifungu cha (2) cha kifungu hiki, Spika ataweka maelezo katika Sheria hiyo kuonesha kuwa Sheria hiyo imekuwa Sheria kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 79(2) cha Katiba."

Kuongeza kifungu kipya cha 80A.

**48.** Katiba inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 80A mara baada ya kifungu cha 80 kama ifuatavyo:-

"Kura ya Maoni kwa mabadiliko ya vifungu vya Katiba.

**80A.**(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 80 cha Katiba, Baraza la Wawakilishi halitaweza kufanya mabadiliko ya Katiba kuhusiana na sharti lolote liliomo katika kifungu chochote kilichoainishwa katika kijifungu cha (2) cha kifungu hiki, mpaka kwanza mabadiliko hayo yakubaliwe na wananchi kwa Kura ya Maoni.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki, vifungu vinavohitaji Kura ya Maoni ni:

(a) vifungu vyote vya Sehemu ya Kwanza ya Sura ya Kwanza;

(b) kifungu cha 9;

(c) vifungu vyote vya Sura ya Tatu;

(d) kifungu cha 26;

(e) kifungu cha 28;

(f) vifungu vyote vya Sehemu ya Pili na Sehemu ya Tatu ya Sura ya Nne isipokuwa kifungu cha 49 na 50;

(g) kifungu cha 80A; na

(h) vifungu vya 121(1) na 123 vya Sura ya Kumi.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya vijifungu vya (1) na (2) vya kifungu hiki, kifungu chochote kilichotajwa chini ya kijifungu cha (2) kinaweza kurekebishwa bila ya kuitisha Kura ya Maoni pale Baraza la Wawakilishi kwa Azimio Maalum lililopitishwa kwa kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wajumbe waliohudhuria na kupiga kura, litaporidhika kwamba marekebisho yanayotaka kufanywa ni ya kiutaratibu, ya kiuandishi ama ya kuweka bayana jambo lenye utatanishi na hayaathiri madhumuni ya msingi ya kifungu husika.

(4) Bila ya kuathiri masharti yaliyoelezwa katika kijifungu cha (2) cha kifungu hiki Kura ya Maoni inaweza kuitishwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi."

Marekebisho ya kifungu cha 81.

**49.** Kifungu cha 81 cha Katiba kinarekebishwa kwa kufuta maneno "Waziri Kiongozi" na badala yake kuweka maneno "Makamo wa Pili wa Rais".

Marekebisho ya kifungu cha 84.

**50.** Kifungu cha 84 cha Katiba kinarekebishwa kwa kufuta maneno "Serikali ya Mapinduzi ya".

Marekebisho ya kifungu cha 86.

**51.** Kifungu cha 86(3) cha Katiba kinarekebishwa kwa kufuta maneno "jukumu lao Barazani au kwengine kokote" na badala yake kuweka maneno "majukumu yao Barazani, katika Kamati za Kudumu za Baraza au katika Kamati Teule za Baraza".

Marekebisho ya kifungu cha 91.

**52.** Kifungu cha 91(2)(e) cha Katiba kinarekebishwa kwa kufuta maneno "Waziri Kiongozi" na badala yake kuweka maneno "Makamo wa Pili wa Rais".

Marekebisho ya kifungu cha 92.

**53.** Kifungu 92(2) cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza maneno "Jamhuri ya Muungano wa" baada ya maneno "Wakati wowote".

Marekebisho ya kifungu cha 96.

**54.** Kifungu cha 96 cha Katiba kinarekebishwa kama ifuatavyo:-

(i) kwa kuongeza maneno "Jaji Mkuu, Kaimu Jaji Mkuu na" mwanzo wa maneno; na

(ii) kwa kufuta maneno "ale kiapo" na kuweka badala yake "aapishwe" na kwa kuongeza maneno "mbele ya Rais" baina ya maneno "chochote" na "kitachowekwa".

Marekebisho ya kifungu cha 99A.

**55.** Kifungu cha 99A(2) cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta neno "Maombi" yaliyopo mwanzo wa Kifungu na kuweka badala yake neno "Rufaa".

Marekebisho ya kifungu cha 102.

**56.** Vifungu vya 102, 102A na 103 vya Katiba vinafutwa na kuandikwa kifungu kipya cha 102 kama ifuatavyo:-

"Tume ya Utumishi ya Mahkama.

**102.** Kutakuwa na Tume ya Utumishi ya Mahkama ambayo muundo, kazi na uwezo wake utakuwa kama ilivyoelezwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi".

Marekebisho ya kichwa cha maneno.

**57.** Katiba inarekebishwa kwa kufuta kichwa cha maneno "Tume ya Utumishi Serikalini" katika "Sura ya Nane" na badala yake kuweka maneno "Kamisheni ya Utumishi wa Umma".

Marekebisho ya kifungu cha 116.

**58** Kifungu cha 116 cha Katiba kinafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

."Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

**116.**(1) Kutakuwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma ambayo itakuwa ni chombo cha juu kabisa kwa Tume zote za Utumishi, chenye mamlaka ya kusimamia na kuratibu mambo yote ya utumishi wa umma kwa Zanzibar.

(2) Muundo, kazi na uwezo wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma itakuwa kama itakavyoelezwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi."

Marekebisho ya kifungu cha 117.

**59.** Kifungu cha 117 cha Katiba kinafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

"Tume ya Utumishi ya Serikali.

**117.** Kutakuwa na Tume ya Utumishi ya Serikali kama itavyoelezwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi."

Marekebisho ya kifungu cha 118.

**60.** Kifungu cha 118 cha Katiba kinafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

"Uwezo wa Tume za Utumishi.

**118.** Bila ya kuathiri masharti ya Katiba, Tume za Utumishi zilizotajwa ndani ya Katiba zitakuwa na mamlaka yafuatayo:

(a) kuajiri watu kushika nafasi za utumishi;

(b) kuthibitisha ajira zao za utumishi;

(c) kusitisha au kuachisha utumishi wao;

(d) kupendekeza Serikalini mishahara na marupurupu ya watumishi wao; na

(e) mamlaka mengine yoyote zitakaopewa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi."

Marekebisho ya kifungu cha 120.

**61.** Kifungu cha 120(4) cha Katiba kinarekebishwa kwa kufuta maneno "Baraza la Wawakilishi litakapoamuru kufanywa hivyo".

Marekebisho ya kifungu cha 121.

**62.** Kifungu cha 121(4) cha Katiba kinarekebishwa kwa kufuta maneno "vikosi vya SMZ" na badala yake kuweka maneno "Idara Maalum".

Marekebisho ya kifungu cha 122.

**63.** Kifungu cha 122 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta neno "Uajiri" yaliyopo baina ya "Tume ya" na "Idara Maalum" na kuweka badala yake neno "Utumishi".

Marekebisho ya kifungu cha 124.

**64.** Kifungu cha 124(2) cha Katiba kinarekebishwa kwa kufuta aya ya (b) na badala yake kuweka aya mpya ya (b) kama ifuatavyo:-

"(b) Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano".

Marekebisho ya kifungu cha 128.

**65.** Kifungu cha 128 cha Katiba kinafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

Serikali za Mitaa.

**128.** Kutakuwa na Serikali za Mitaa ambazo uchaguzi wa viongozi wake, madaraka na kazi za kila Serikali ya Mtaa zitakuwa kama zitavyoelezwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi."

Marekebisho ya kifungu cha 129.

**66.** Kifungu cha 129 cha Katiba kinarekebishwa kama ifuatavyo:-

(i) kwa kufuta maneno "kwa maandishi ya mkono wake" na kuweka badala yake "kwa maandishi aliyoweka saini yake" katika kijifungu cha (1).

(ii) kwa kufuta neno "Jaji Mkuu" na badala yake kuweka neno "Spika" katika kijifungu cha (3);

(iii) kwa kufuta kijifungu cha (4) na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

"(4) Taarifa ya kujiuzulu kwa Makamo wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais, Waziri, Naibu Waziri na Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi itapelekwa kwa Rais;"

(iv) kwa kufuta kijifungu cha (5) na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

"(5) Taarifa ya kujiuzulu kwa Spika, itapelekwa Baraza la Wawakilishi;"

(v) kwa kufuta kijifungu cha (6) na badala yake kuandikwa upya kama ifuatavyo:

"(6) Taarifa ya kujuizulu kwa Naibu Spika, au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi itapelekwa kwa Spika."

Marekebisho ya kifungu cha 134.

**67.** Kifungu cha 134(1) cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

(i) kwenye ufafanuzi wa "Waziri" kwa kufuta neno "Memba" na kuweka badala yake neno "Mjumbe";

(ii) kwa kuongeza ufafanuzi wa "Utumishi wa Umma" kama ifuatavyo:-

"Utumishi wa Umma" maana yake ni ajira katika utumishi unaosimamiwa moja kwa moja na Tume ya Utumishi Serikalini, Tume ya Utumishi ya Mahkama, Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi, Tume ya Utumishi ya Idara Maalum na inajumuisha utumishi katika taasisi zinazojitegemea ambazo zinafanya kazi za Serikali au zinamilikiwa na Serikali na kadri tafsiri itavyohitaji, inajumuisha utumishi katika mashirika ya kibiashara yanayomilikiwa na Serikali. Isipokuwa kwamba haitajumuisha utumishi wa kisiasa na utumishi wa maofisa ambao Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi kwa masharti ya wazi imewaondoa katika tafsiri ya utumishi wa umma.

**IMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi tarehe 9 mwezi wa Agosti, 2010.

**(IBRAHIM MZEE IBRAHIM)**
**KATIBU**
**BARAZA LA WAWAKILISHI**